# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA AFYA

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU TISHIO LA MLIPUKO WA UGONJWA WA EBOLA

**DAR ES SALAAM, 28 Septemba, 2022**

**Ndugu Wananchi,** Siku ya tarehe 20 Septemba, 2022 Wizara ya Afya ilipokea taarifa iliyotolewa na Waziri wa Afya wa Uganda, kupitia vyombo mbalimbali vya habari juu ya mlipuko wa ugonjwa wa Ebola katika Wilaya ya Mubende nchini humo. Wilaya ya Mubende iko umbali wa takribani kilometa 130 hadi Kampala, Makao Makuu ya Uganda. Kutoka Kampala hadi Mutukula Mkoani Kagera Tanzania ni umbali wa takribani kilometa 220. Aidha kutoka Mubende kwenda Mutukula, Mkoani Kagera Tanzania kupitia Masaka ni umbali wa kilomita 230.

Ndugu wananchi, hadi kufikia tarehe 26 Septemba, 2022, jumla ya **wagonjwa 43 na vifo 23 vimetolewa taarifa**. Taarifa zinaonesha kuwa watu hawa wana dalili za homa kali, degedege, kutapika matapishi yenye damu, kuharisha na kutokwa damu machoni. Uchunguzi wa kimaabara umethibitisha kuwepo kwa ugonjwa wa Ebola anuai aina ya Sudan (Ebola-Sudan strain). Hadi sasa jumla ya watu 425 waliotangamana na wagonjwa (Contacts) wameanishwa na kati yao watu 127 wamepatikana na wanafuatiliwa ikiwa wataonyesha dalili za kuwa na ugonjwa huu.

**Ndugu Wananchi,** Uwepo wa ugonjwa wa Ebola katika nchi jirani unaiweka nchi yetu katika hatari kubwa kutokana na mwingiliano mkubwa wa shughuli za kiuchumi na kijamii kupitia mipaka rasmi na isiyo rasmi. **Uchambuzi wetu umeonyesha kuwa Mikoa iliyo hatarini zaidi ni Kagera, Mwanza, Kigoma, Geita na Mara**. Aidha Mikoa ya Dar es salaam, Arusha, Kilimanjaro, Songwe, Mbeya na Dodoma ipo katika hatari kwa sababu ya uwepo wa viwanja vya ndege na vituo vikubwa vya mabasi ya kutoka nchi jirani. **Hata hivyo, hadi sasa hakuna mgonjwa wa Ebola nchini Tanzania.** Hivyo yatupasa kila mmoja wetu kuchukua hatua na kuhakikisha ugonjwa huu hauingii nchini.

Ugonjwa wa Ebola uligundulika kwa mara ya kwanza mwaka 1976 katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Sudan. Tangu kugundulika kwake, kumekuwa na milipuko kadhaa katika nchi za Uganda na DRC ambapo DRC imekuwa na milipuko mingi zaidi. Nchi za Uganda na DRC tunapakana nazo.

**Ndugu Wananchi**, Ugonjwa wa Ebola unasababishwa na Kirusi aina ya Ebola chenye anuwai tano zikiwemo anuwai za *Zaire* na *Sudan* ambazo ndiyo zinasababisha milipuko. Ugonjwa huu hutokea kwa nadra lakini una madhara makubwa sana. **Dalili kuu za ugonjwa huu ni homa kali, mwili kuchoka, kuumwa viungo vya mwili, vidonda katika koo, kuhara, na kutokwa damu katika matundu ya mwili yaani puani, mdomoni, masikioni, machoni na njia ya haja kubwa na ndogo** hali inayopelekea kifo ndani ya muda mfupi.

**Ndugu Wananchi**, Ugonjwa huu ni miongoni mwa magonjwa yanayosambaa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu kwa kula au kugusa mnyama mwenye maambukizi. Wanyama hao ni kama vile Nyani, Kima, Popo na Swala. Unaenea kutoka kwa binadamu mmoja hadi mwingine kwa kugusa majimaji ya mwili wa mgonjwa kwa mfano mate, machozi, damu, matapishi, mkojo na kinyesi. **Endapo mtu yoyote atapata au kuona mtu mwenye dalili hizi, anashauriwa kuwahi kituo cha kutolea huduma za afya mapema** kwa ajili ya uchunguzi na matibabu.

**Ndugu Wananchi,** Hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa na Serikali ili kuzuia ugonjwa kuingia nchini ikiwemo kuimarisha utayari wa kukabiliana na ugonjwa kwa kufanya yafuatayo:

a) Kamati ya Kitaifa ya Wataaluma ya kukabiliana na Magonjwa ya Milipuko (National Task Force on Public Health Events) inayojumuisha wataalamu kutoka sekta mbalimbali imeitishwa ili kuratibu na kusimamia utayari wa nchi wa kukabiliana na ugonjwa huu,
b) Kuimarisha timu za haraka za uratibu (Rapid Response Team) ngazi zote ikiwa pamoja na kuanza kufanya mafunzo kwa timu mbalimbali za wataalam
c) Kuhakikisha dawa, vifaa na vifaa tiba muhimu vinakuwepo katika vituo vya kutolea huduma za afya hususani mkoani Kagera

d) Kuelimisha na kuhamasisha jamii kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huu,
e) Kuimarisha uchunguzi wa wasafiri katika mipaka hasa yenye mwingiliano mkubwa na nchi ya Uganda- Mutukula, Dar es salaam, Kilimanjaro, Kigoma na Mara.
f) Kuimarisha ufuatiliaji wa tetesi za watu wenye viashiria vya ugonjwa kwenye jamii na vituo vya kutolea huduma za afya kote nchini
g) Kuhakikisha uwepo wa vituo vya kuwahudumia wagonjwa watakao thibitika
h) Kuimarisha mfumo wa usafirishaji wa sampuli kwa ajili ya kufikisha katika maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii Dar es salaam.
i) Kuimarisha huduma za upimaji katika Mkoa wa Kagera kwa kuweka huduma ya Maabara tembezi.

**Ndugu Wananchi,** Kutokana na tishio la kupata mlipuko wa ugonjwa wa Ebola nchini na kupitia mamlaka niliyopewa chini ya Sheria ya Afya ya Jamii (Public Health Act) ya mwaka 2009 kifungu cha 4 (1) ninaelekeza Wakuu wa Mikoa yote nchini kusimamia yafuatayo katika Mikoa yao:

a) Kila Mkoa na Halmashauri kuandaa mpango (Contigency Plan) wa kukabiliana na mlipuko wa ugonjwa huu
b) Kuimarisha ufuatiliaji (surveillance) na kutoa taarifa ya wahisiwa wenye dalili za ugonjwa wa Ebola katika maeneo yao kupitia Mfumo wa Magonjwa ya Mlipuko na yanayopewa kipaumbele (IDSR). Aidha, kuhakikisha Waganga Wakuu wa Mikoa wanatoa Taarifa sahihi na kwa wakati kwa Mganga Mkuu wa Serikali kuhusu tetesi za wahisiwa na mwenendo wa ufuatilia wa ugonjwa huu.
c) Kufuatilia ukaguzi wa afya za wasafiri wanaoingia nchini hususani kutoka nchi zilizoathirika.
d) Kuimarisha timu za haraka za kukabiliana na magonjwa ya mlipuko (Rapid Response Team) ndani ya Mikoa yao
e) Kutoa elimu kwa wananchi juu ya ugonjwa huu na namna ya kujikinga
f) Kuandaa/Kuimarisha vituo vya matibabu ya wagonjwa kwa kila Halmashauri
g) Kuhakikisha uwepo wa dawa, vifaa tiba na kinga kwa ajili ya wagonjwa
h) Kuhakikisha uwepo wa vifaa kinga (PPE) kwa ajili ya watumishi wa afya katika maeneo yote muhimu
i) Kuandaa maeneo maalum ya kuweka wahisiwa (Contacts)

j) Kubainisha eneo maalum la maziko katika Halmashauri zote
k) Kuhakikisha kuwa kunakuwa na miundombinu ya kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni au kwa kutimia vitakasa mikono katika ngazi ya kaya, Taasisi, Sehemu za biashara, stendi za mabasi, mashuleni, nyumba za ibada na maeneo yenye mikusanyiko ya

**Ndugu Wananchi,** Aidha ili kujikinga na ugonjwa huu, ninawataka wananchi kuchukua hatua zifuatazo:

a) Kuepuka kutembelea maeneo yenye ugonjwa wa Ebola,
b) Kuepuka kula nyama ambayo haijapikwa vizuri, kula nyama mbichi au mizoga na kugusa mnyama mgonjwa,
c) Kuepuka kugusa majimaji ya mwili wa mtu mwenye dalili za ugonjwa wa Ebola kwa mfano mate, machozi, damu, mkojo na kinyesi,
d) Kunawa mikono mara kwa mara unapotembelea wagonjwa,
e) kujenga utamaduni wa kunawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono.

**Ndugu wananchi,** Nihitimishe kwa kutoa rai kwa kila mmoja wetu kuendelea kuchukua tahadhari za kuhakikisha ugonjwa huu hauingia nchini kwetu. Wizara itaendelea kufuatilia na kutoa taarifa juu ya ugonjwa huu mara kwa mara.

***Chukua Hatua Mapema, Ebola Inazuilika, Kinga ni Bora kuliko Tiba!***

Imetolewa na;

Ummy A. Mwalimu (Mb)

**WAZIRI WA AFYA**